

Nukuu za maisha

"Maisha ni ama tukio la kuthubutu lenye kusi-simua au si chochote kabisa. Usalama haupo kati-ka asili, wala haupatikani kwa kujificha kila wakati... Kuepuka hatari si salama zaidi kwa muda mrefu kuliko kujikabili nayo moja kwa moja, kwa ujasiri unaosukumwa na matumaini ya kesho iliyo bora zaidi." **Hellen Keller**



"Dhamira yangu maishani si kuishi tu, bali kust-awi; na kufanya hivyo kwa shauku, huruma, ucheshi, na mtindo wa kipekee, huku nikigusa maisha ya wengine kwa njia chanya, yenye maana, na ya kudumu." **Maya Angelou**



"Ni rahisi zaidi kujenga watoto imara kuliko kurekebisha wanaume waliovunjika, kwa sababu msingi wa tabia hujengwa mapema kupitia malezi yenye maadili, upendo, nidhamu, na mwongozo wa wazazi wanaojali." **Fredrick Douglas**



"Upendo na huruma ni msingi wa malezi bora; bila hivyo, watoto hukua bila mwelekeo wa kweli wa maisha, hivyo ni muhimu kuwafundisha maadili, uvumilivu, na kujali wengine tangu wakiwa wadogo." **Dalai Lama**

Agizo vibali vya ujenzi kwa sharti la kupanda miti lipewe uzito

Juzi, dunia iliadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, na Tanzania ikiadhimisha jijini Dodoma kwa kujadili na kutoa tathmini ya hali ya mazingira kwa sasa. Agizo la Makamu wa Rais, Dk Emmanuel Nchimbi alilolitoa kwenye maadhimisho hayo, kwamba vibali vya ujenzi vitakavyotolewa nchini viwe na sharti la kupanda miti, ni moja ya uamuzi muhimu unaoweza kuleta mabadiliko makubwa katika uhifadhi wa mazingira iwapo litatekelezwa kwa umakini na usimamizi wa kutosha.

Dk Nchimbi alitoa agizo hilo akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye maadhimisho hayo. Kauli hiyo imekuja wakati ambao dunia inaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la joto duniani, ukame, mafuriko na uharibifu wa mazingira unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu.

Kwa maoni yetu, agizo hili halipaswi kubaki kuwa tamko la siku moja la maadhimisho ya mazingira. Badala yake, mamlaka zote zinazohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi zinapaswa kuliingiza rasmi katika masharti ya lazima kwa kila anayeomba kibali cha kujenga nyumba, jengo la biashara,

ra, taasisi au aina yoyote ya miundombinu.

Vilevile, uwepo wa miti katika maeneo ya ujenzi unapaswa kuwa sehemu ya ukaguzi wa maendeleo ya mradi husika.

Kwa miaka mingi, kasi ya ukuaji wa miji na makazi imekuwa ikiambatana na kupungua kwa maeneo ya kijani. Maeneo mengi ambayo zamani yalikuwa na miti mingi sasa yamegeuzwa kuwa makazi au maeneo ya biashara bila juhudi za kutosha za kurejesha uoto wa asili.

Matokeo yake ni kuongezeka kwa joto, kupungua kwa ubora wa hewa na kuongezeka kwa athari za mazingira ambazo mwishowe huathiri maisha ya wananchi.

Ni ukweli usioplingika kwamba miti ina mchango mkubwa katika kuboresha mazingira. Husaidia kufyonza hewa ya ukaa, kutoa oksijeni, kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuhifadhi vyanzo vya maji na kupunguza joto katika maeneo ya makazi. Aidha, miti huongeza uzuri wa mazingira na kufanya maeneo ya makazi kuwa bora zaidi kwa afya na ustawi wa wananchi.

Hata hivyo, tunashauri utekelezaji wa agizo hili usijikite katika kupanda miti ya kivuli pekee. Kuna umuhimu mkubwa wa kuhamasisha upandaji wa

miti ya matunda ambayo mbali na faida za kimazingira, pia ina manufaa ya kiuchumi na kijamii. Miti kama maembe, maparachi-chi, machungwa, mapera, minazi na aina nyingine zinazostawi katika maeneo mbalimbali nchini inaweza kuwa chanzo cha chakula na kipato kwa familia nyingi.

Kupanda miti ya matunda kutasaidia kuongeza upatikanaji wa lishe bora katika jamii, huku baadhi ya wananchi wakipata fursa ya kuuza mazao hayo na kuongeza kipato chao.

Hivyo, badala ya kuona upandaji miti kama jukumu la mazingira pekee, wananchi wanaweza kuliona pia kama uwekezaji wenye manufaa ya moja kwa moja katika maisha yao.

Tunatoa wito kwa halmashauri, wataalamu wa mazingira, mamlaka za mipango miji na serikali za mitaa kuhakikisha agizo hili linatekelezwa kwa vitendo. Aidha, wananchi wanapaswa kulipokea kwa moyo chanya na kulifanya kuwa sehemu ya utamaduni wa maendeleo ya makazi yao.

Ikiwa kila jengo jipya litakwenda sambamba na upandaji na utunzaji wa miti, Tanzania itakuwa imepiga hatua kubwa katika kujenga mazingira salama, yenye afya na endelevu.

Wazazi tuwe macho dawa za kulevya zikiharibu wanafunzi

Tafiti zinaonyesha kuwa matumizi ya bangi katika kipindi cha ujana yanaweza kuathiri uwezo wa kufikiri, kukumbuka na kuchakata taarifa.



Elizabeth Edward | **Uwanja wa mwanamke**

Kwa mzazi anayejitolea kila kitu ili mwanawe afike chuo kikuu, ndoto yake huwa ni kumuona akihitimu na kupata maisha bora.

Lakini nyuma ya kuta za baadhi ya vyuo na taasisi za elimu ya juu, kuna vita nyingine inayotishia ndoto hizo matumizi ya dawa za kulevya, hususan bangi na skanka, ambayo imekuwa ikiwavuta vijana wengi katika mzunguko wa utegemezi, kushuka kitaaluma na wakati mwingine kuharibu kabisa mustakabali wao.

Wakati jamii nyingi zikiamini kuwa tatizo la dawa za kulevya linawahusu zaidi watu wazima, hali halisi inaonyesha vijana ndio wamekuwa wahanga wakubwa.

Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025 inaonyesha kuwa matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo yanaongezeka na kusababisha madhara makubwa ya kiafya, kijamii na kiuchumi, huku baadhi ya vijana wakianza kutumia dawa hizo wakiwa bado shule za sekondari na kuendelea nazo wanapoingia vyuoni.

Matukio ya wanafunzi wa vyuo vikuu kukamatwa au kuhusishwa na matumizi ya bangi na skanka yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara katika maeneo mbalimbali.

Wengi huingia katika matumizi hayo kwa ushawishi wa marafiki, kutaka kujionyesha kuwa wa kisasa au kwa imani potofu kwamba dawa hizo huwasaidia kupunguza msongo wa mawazo na kuongeza uwezo wa kujifunza.

Hata hivyo, wataalamu wanaonya kuwa dhana hizo ni za kupotosha na mara nyingi huwa mwanzo wa matatizo makubwa zaidi.

Takwimu za kimataifa zinaonyesha ukubwa wa changamoto hiyo. Katika eneo la Oceania linalojumuisha Australia, New Zealand na Visiwa vya Pasifiki, matumizi ya bangi miongoni mwa wanafunzi wa miaka 15 na

16 yanafikia asilimia 13, kiwango cha juu zaidi kuliko wastani wa dunia wa asilimia 4.4.

Barani Ulaya, matumizi ya bangi kwa vijana wa umri huo bado ni makubwa kuliko ilivyo kwa watu wazima, hali inayonyesha kuwa vijana ndio kundi linalobeba mzigo mkubwa wa tatizo hilo.

Ingawa takwimu hizo zinatoka nje ya Tanzania, zinaonyesha namna dawa za kulevya zinavyoendelea kupenya katika maisha ya wanafunzi duniani kote.

Kwa upande wa vyuo vikuu, bangi na hasa skanka zimekuwa maarufu zaidi kutokana na uwezo wake wa kusababisha ulevi mkali kwa muda mfupi.

Tatizo ni kwamba watumiaji wengi huanza kwa majaribio wakiamini wanaweza kuacha wakati wowote. Baada ya muda, matumizi hayo hugeuka kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku na kuathiri uwezo wao wa kufanya maamuzi sahihi.

Athari za dawa hizo kwa mwanafunzi ni kubwa kuliko wengi wanavyofikiri. Tafiti zinaonyesha kuwa matumizi ya bangi katika kipindi cha ujana yanaweza kuathiri uwezo wa kufikiri, kukumbuka na kuchakata taarifa.


Kwa mwanafunzi wa chuo kikuu anayehitaji umakini wa hali ya juu katika masomo, hali hiyo inaweza kusababisha kushuka kwa ufaulu, kuongezeka kwa uoto na hata kushindwa kuhitimu kwa wakati. Mbali na kuathiri masomo, matumizi ya bangi na skanka yanaweza kuvuruga maendeleo ya binafsi na kitaaluma.

Vijana wengi wanaojihusisha na dawa hizo hujikuta wakipoteza motisha ya kujifunza, kushindwa kupanga malengo ya maisha na kupunguza uwezo wao wa kutumia kikamilifu fursa zinazopatikana katika elimu na ajira.

Changamoto nyingine kubwa ni afya ya akili. Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025 inaeleza kuwa matumizi ya mara kwa mara ya bangi, hasa yanapoanza katika umri mdogo, yanaweza kuongeza hatari ya kuchanganyikiwa, matatizo ya hisia na wasiwasi.

Katika mazingira ya vyuo vikuu ambako tayari kuna shinikizo la masomo na maisha ya kujitegemea, matumizi ya dawa hizo yanaweza kuongeza zaidi matatizo ya kisaikolojia.

KING KINYA



HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LIMITED (MCL)

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam
+255 22 24 50875, 0754 780647, 0765 864917
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Rosalynn Mndolwa-Mworia: Mkurugenzi Mtendaji
Mpoki Thompson: Mhariri Mtendaji Mkuu
Joseph Damas: Mhariri Mtendaji

Tunawezesha taifa